ANDIKO LA KISERA

MEI 2018

# Kutekeleza Awamu ya Pili ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa Kupitia Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki

UJUMBE MUHIMU

- Utekelezaji wa miradi ya uhifadhi katika safu za Milima ya Tao la Mashariki iliyoko upande wa Tanzania ulichangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo ya maendeleo kitaifa na katika ngazi za chini.
- Kuwekeza katika uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki kuna manufaa mengi kwa mazingira na kwa uchumi wa taifa, ikiwamo kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kufanikisha utekelezaji wa awamu ya pili ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ya Taifa.

## Utangulizi na Maelezo kwa ufupi

Ikiwa imetambaa kuanzia Kusini mwa Tanzania mpaka Kusini-Mashariki mwa Kenya, ikiwa na ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 23,000 za safu za milima, Milima ya Tao la Mashariki ni milima ya tangu enzi na enzi – inayoundwa na Milima ya Upare (Kaskazini na Kusini), Usambara (Magharibi na Mashariki), Nguu, Nguru, Ukaguru, Uluguru, Malundwe, Rubeho, Udzungwa na Mahenge kwa upande wa Tanzania, na Vilima vya Taita kwa upande wa Kenya. Umuhimu wa Milima hii kama kitovu cha bioanuwai ya ulimwengu na umuhimu wake katika kutoa huduma mbalimbali ni dhahiri – hivyo kuwa yenye kipaumbele cha uhifadhi kitaifa na kimataifa, ikihitaji ufadhili wa muda mrefu, wa uhakika na endelevu. Mfuko wa Hifadhi za Milima ya Tao la Mashariki 'Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund (EAMCEF)' ulianzishwa na serikali mnamo Juni 2001 kama mfuko wa udhamini ambao utapitisha fedha/ufadhili ili kuhakikisha uhifadhi wa muda mrefu wa mfumo wa ikolojia wa Milima ya Tao la Mashariki. Mnamo Juni 2011, Serikali ya Norway ilitoa ruzuku ya mradi yenye thamani ya Dola za Kimarekani Milioni 5.95 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa miaka mitano (2011-2016) wa kuboresha uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki uliolenga Maeneo ya Hifadhi tisa yaliyopewa kipaumbele; maeneo manane yakiwa ni Misitu ya Hifadhi za Asili - Amani, Nilo, Magamba, Chome, Uluguru, Mkingu, Kilombero, Uzungwa Scarp, na moja likiwa ni Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa. Maeneo haya ya hifadhi yamo ndani ya mamlaka za Wilaya 11 za Mkinga, Muheza, Korogwe, Lushoto, Same, Mvomero, Morogoro, Manispaa ya Morogoro, Kilombero, Kilolo na Mufindi. Mradi huu wa miaka mitano uliotekelezwa na EAMCEF ulileta matokeo makubwa ambayo yalishawishi kupata ufadhili wa kuendeleza mradi kwa awamu nyingine ya pili, kuanzia 2016-2019 kwa bajeti ya Dola za Kimarekani Milioni 3.125.

Andiko hili linaonyesha namna ambavyo matokeo ya mradi wa EAMCEF yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kufikia malengo ya awamu ya kwanza ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa (unaofupishwa kwa Kiingereza kama FYDP I), pamoja na kuonyesha ni kwa namna gani mradi uliopo sasa (2016-2019) unavyoweza kuchangia katika kufikia malengo ya awamu ya pili ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa (unaofupishwa kwa Kiingereza kama FYDP II).

## Uhusiano wa Mradi wa EAMCEF na Mipango ya Maendeleo ya Taifa

Awamu ya kwanza ya mradi wa EAMCEF (2011-2016) unaendana vyema na muda wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo wa Taifa (FYDP I) uliotekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2011/12 - 2015/16. Kwa mantiki hiyo, mchango wa matokeo ya mradi wa EAMCEF unaweza kuhusianishwa kwa urahisi na utekelezaji wa FYDP I, na wakati huo huo ukiwa wa muhimu katika kufikia azima ya FYDP II (2016/17 – 2020/21). Mipango yote miwili ya maendeleo ya Taifa inahamasisha jitihada za pamoja na za binafsi katika kuibadilisha Tanzania kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Ufuatao ni muhtasari wa namna gani mradi wa EAMCEF umechangia na unahusiana na Mipango yote miwili ya Miaka Mitano ya Maendeleo ya Taifa (FYDP I na FYDP II).

## Mchango wa mradi wa EAMCEF katika utekelezaji wa FYDP I (2011/12 - 2015/16)

### Kilimo Kinachoendana na Mabadiliko ya Tabianchi

**SHUGHULI MUHIMU**

- Usimamizi jumuishi wa ardhi na udongo
- Kuimarisha vyama na vikundi vya wakulima
- Hamasisha kilimo cha mazao yenye ubora wa juu, ikiwamo mazao ya miti ya viungo...matunda, mbogamboga...

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Mradi wa EAMCEF ulianzisha kilimo hifadhi – aina ya kilimo kinachohifadhi maji kwa kupunguza kasi ya maji yanayotiririka mashambani, kwa kuzuia mmomonyoko wa udongo unaosababisha rutuba kupotea.
- Mradi ulitoa mafunzo ya kilimo hifadhi kwa wanavijiji 329 katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Manispaa ya Morogoro – mpaka kufikia mwishoni mwa mradi, tayari jumla ya kaya 686 zilishapokea kilimo hifadhi kwa kulima jumla ya hekari 863.
- Mbinu hii ya kilimo hifadhi imeongeza uzalishaji wa mazao mara mbili mpaka tatu zaidi kwa ekari moja, hivyo kuweka uhakika wa usalama wa chakula na kuongeza kipato.
- Mradi ulikuza uzalishaji wa matunda na mbogamboga kwa kutoa mafunzo kwa wanavijiji 711 wa Wilaya za Mkinga, Mufindi na Manispaa ya Morogoro. Wanavijiji 517 walipatiwa pembejeo. Mradi pia ulisaidia vikundi vya wakulima wa mbogamboga.
- Kuhusu kilimo cha miti ya viungo, katika Wilaya ya Muheza mradi wa EAMCEF ulitoa mafunzo kwa wanawake 55 na

kuanzisha vitalu vitatu ya miche, na kupanda hekari 27.

- Uuzaji wa miche ya miti ya viungo ulileta mapato ya Tsh. 9,700,000 na kuwezesha wakulima kukidhi mahitaji ya kimaisha ya kila siku.

## Shughuli za Uvuvi



**SHUGHULI MUHIMU**

- Wezesha uendelezaji wa maeneo yenye maji

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Mradi ulianzisha ufungaji wa samaki katika Wilaya ya Kilolo kama sehemu mojawapo ya shughuli mbadala za kujipatia kipato na chanzo cha protini kwa kutoa mafunzo kwa wanavikijiji 322.
- Jamii zilizoshiriki zilipatiwa vifaa vya kuanzisha ufugaji wa samaki, jumla ya mabwawa 97 yalianzishwa, jumla ya samaki 12,155 walivunwa.

## MISITU



**SHUGHULI MUHIMU**

- Usimamizi endelevu wa rasilimali za misitu
- Usimamizi endelevu wa rasilimali za nyuki

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Mradi ulifadhili miradi ya uhifadhi wa misitu katika Maeneo ya Hifadhi tisa kupitia ruzuku iliyowezesha shughuli za kila siku za uendeshaji wa maeneo hayo – kama vile, usafishaji wa mipaka, ukaguzi na uwekaji alama za mipaka, doria za misitu, uanzishwaji wa njia za matembezi na barabara za utalii.
- Usimamizi wa misitu ulikwenda sambamba na kukabiliana na vyanzo vya uharibufu wa misitu na ukataji miti ovyo kupitia ushirikishwaji mkubwa wa wanajamii, pamoja na kusaidia jamii kufanya shughuli mbadala za kujipatia kipato.
- Kwa ujumla, shughuli za usimamizi wa misitu pamoja na ukarabati wa maeneo yaliyoharibiwa umesaidia kuota upya kwa msitu kwa kiasi cha hekta 1,000.
- Mradi ulisaidia shughuli za ufugaji nyuki kama chanzo mbadala cha shughuli za kujipatia kipato katika maeneo yote ya misitu yaliyokuwa yamepewa kipaumbele na mradi, mradi ulitoa mafunzo kwa wanavijiji 1, 570 juu ya mbinu za kisasa za ufugaji nyuki. Jumla ya vikundi 82 viliundwa.
- Msaada kutoka kwenye mradi ulikuwa: ununuzi wa mizinga ya kisasa 1, 274, mashine 37 za kukamua asali pamoja na vifaa vingine vya shughuli za ufugaji nyuki.

## Mifugo



**SHUGHULI MUHIMU**

- Kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wa kisasa wa maziwa.
- Kuongezeka kwa uzalilishaji wa maziwa
- Kuongezeka kwa uzalishaji wa mayai

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Mradi ulisaidia shughuli za ufugaji mifugo – mbuzi wa maziwa kwa Manispaa ya Morogoro Mjini, na katika Wilaya za Mkinga na Kilolo.
- Mafunzo yalitolewa kwa wanavijiji 314 na kupewa jumla ya mbuzi wa maziwa 226.
- Watoto wa mbuzi 130 walizaliwa na kugawiwa kwa kaya za jirani kama sehemu ya kueneza manufaa ya mradi.
- Vile vile, mradi ulianzisha shughuli za ufugaji wa ng'ombe wa maziwa (na ufugaji wa nguruwe) katika Wilaya ya Kilolo na kutoa mafunzo kwa wanavijiji 50 na kisha kugawa ng'ombe 20 ili kuanzisha ufugaji.
- Kupitia ng'ombe wa maziwa, jamii zimeweza kujihakikishia upatikanaji wa maziwa ya ziada kwa ajili ya matumizi ya kaya na kujipatia kipato kupitia uuzaji wa maziwa na nyama.
- EAMCEF ilifadhili ufugaji wa kuku wa kienyeji walioboreshwa kwa jamii ya Wilaya za Korogwe, Same na Mvomero. Mradi ulitoa mafunzo kwa wanavijiji 873 na kuwapatia kuku 2,061 waliogawiwa kwa kaya 439.

## Utalii



**SHUGHULI MUHIMU**

- Tambua na boresha maeneo ya vivutio vya utalii na bidhaa zake.
- Endeleza uhifadhi endelevu na usimamizi wa maeneo ya kitamaduni.
- Kuza uwezo wa taasisi za usimamizi wa wanyamapori.
- Uhifadhi, utunzaji na utangazaji wa rasilimali za urithi wa kitamaduni.
- Uhusishwaji wa jamii na ushiriki katika uhifadhi wa urithi wa kitamaduni pamoja na kuendeleza na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi.

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa maeneo ya hifadhi 9 kupitia ufadhili uliowezesha kuweka alama katika mipaka, kusafisha na kupitia upya mipaka, doria za misitu na uzuiaji wa shughuli haramu katika misitu.

- Katika utalii, mradi wa EAMCEF ulisaidia uanzishwaji wa njia za kutembea na barabara za utalii zenye jumla ya urefu wa kilomita 90 katika Hifadhi ya Asili ya Kilombero, kilomita 72 katika Hifadhi ya Nilo, zaidi ya kilomita 50 katika hifadhi za Magamba na Chome, na zaidi ya kilomita 300 katika Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa – ikiwa ni jumla ya zaidi ya kilomita 700 za barabara za kutembea kwa miguu na 177 za kuendesha kwa magari ambazo zote ni muhimu kwa shughuli za utalii.
- Mradi ulifadhili uanzishwaji wa maeneo ya kuweka kambi za watalii 31 katika maeneo ya hifadhi, na pia kusaidia kutangaza maeno hayo kupitia vipindi vya televisheni na redio, pamoja na uandaaji wa vitini vya taarifa na mawasiliano, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji na utumiaji wa tovuti.
- Ufadhili wa shughuli mbalimbali katika maeneo ya hifadhi ulichangia katika kuongeza pato la kila mwaka kitokanacho na utalii.

## Mafanikio ya mradi wa EAMCEF na umuhimu wake katika kufikia malengo ya FYDP II (2016/17 – 2020/21)

| | FYDP II – Maeneo ya kimkakati/malengo ya utekelezaji ili kuboresha uzalishaji yanayoendana na mradi wa EAMCEF | Uhusiano/na mchango wa mradi wa EAMCEF |
|---|---|---|
| Malengo | Wezesha ukuaji jumuishi wa kiuchumi ambao unasaidia kupunguza umasikini kwa kiasi kikubwa...kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji na kutengeneza fursa za ajira, hasa hasa kwa vijana na makundi yasiyopewa kipaumbele. | • Katika ngazi ya lengo, mradi wa EAMCEF una lengo la kufanya shughuli za uhifadhi zinazoendana sambamba na kuboresha maisha ya jamii za pembezoni mwa maeneo ya hifadhi.<br>• Mradi ulisaidia jamii kupata kipato cha ziada kupitia ufanyaji wa shughuli mbadala za kujiingizia kipato, kupitia ajira za vibarua katika usimamizi wa misitu – zilizoajiri vijana, wanaume na wanawake. |
| | Boresha hali ya maisha na ustawi wa watu. | • Kipato walichojipatia wanajamii kupitia ushiriki wao katika shughuli mbalimbali za miradi iliyofadhiliwa na EAMCEF kimewasaidia kuboresha hali zao za maisha – kwa mfano kwa kujenga nyumba bora, kwa kutumia nishati ya kisasa ya gesi itokanayo na wanyama, ujenzi wa madarasa ya wanafunzi na ofisi za walimu. |
| | Imarisha uwezo wa majukumu ya wadau wa ngazi za chini katika kupanga na kutekeleza. | • Muundo wa kitaasisi na kisheria wa usimamizi wa mradi wa EAMCEF ulichangia katika kukuza uwezo wa jamii wa kubuni, kutekeleza na kufuatilia miradi.<br>• Upatikanaji wa watekelezaji wa miradi ulihitaji uidhinishwaji wa madodoso katika ngazi mbalimbali za utawala katika Mikoa na Wilaya, lakini pia muundo huu uliwezesha kujenga ubia na mashirikiano miongoni mwa taasisi za serikali na taasisi zisizo za serikali na zile za kijamii.<br>• Uundwaji wa vikundi mbalimbali vya wanajamii- kama vile vya ufugaji nyuki, vipepeo, kamati za ushauri, kilimo hifadhi, ufugaji samaki, majiko bora – ulichangia sana katika kuinua uwezo wa jamii husika. |
| | hakikisha kuwa makubaliano ya kimataifa na kikanda (kama vile Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu) yanaingizwa kikamilifu katika mfumo wa kitaifa wa mipango na utekelezaji kwa manufaa ya nchi. | • Utaratibu wa utekelezaji wa mradi wa EAMCEF ulijenga (na umejenga) mazingira wezeshi kwa ajili ya uingizwaji rasmi wa masuala mbalimbali katika mfumo wa utekelezaji, kwa mfano uingizwaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (Sustainable Development Goals) katika mipango ya Wilaya. Miradi mbalimbali iliyotekelezwa chini ya usimamizi wa EAMCEF ilijumuishwa katika mipango ya Wilaya husika, na waajiriwa katika Wilaya hizo walihusishwa katika uandaaji na utekelezaji wa miradi, walitoa ushauri wao wa kitaalamu na kushiriki katika ufuatiliaji wa miradi. Mradi wa EAMCEF umechangia (na unaendelea kuchangia) katika juhudi za kufikia malengo kadhaa ya Maendeleo Endelevu – kama vile Lengo namba- 1, 2, 5, 6, 7, 13, and 15 |

## Katika ngazi ya shughuli za kimkakati

### Sekta ya Uzalishaji Viwandani



**SHUGHULI MUHIMU**

- mpango umependekeza kufikia shabaha kwa kutekeleza shughuli mbalimbali za viwandani, ikiwamo kukuza matumizi ya makaa ya mawe kama nishati mbadala ya kuni na mkaa kwa matumizi ya viwanda na majumbani, ili kulinda misitu.

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Kuhusu nishati katika kaya, mradi ulianzisha matumizi ya majiko bora yenye ufanisi zaidi pamoja na matumizi ya gesi itokanayo na wanyama (biogas) ili kupunguza matumizi ya kuni. Mradi ulitoa mafunzo ya kujenga majiko bora kwa mafundi mchundo 1,531 wanaotoka maeneo husika, jumla ya kaya 14,016 zimeshaanza kutumia majiko hayo.
- Kuhusu gesi, jumla ya wanajamii 97 walipewa mafunzo ya kujenga mitambo ya kuzalisha gesi kupitia kinyesi cha wanyama na kusaidia kaya 12 kupata mitambo ya kuzalisha gesi na hivyo kupunguza asilimia 50 ya matumizi ya kuni kwa wiki.

## Kilimo



**SHUGHULI MUHIMU**

- Kukuza mbinu katika mnyororo mzima wa kuongeza thamani
- Kuwezesha vikundi vya wazalishaji

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Mradi ulitoa mafunzo ya mbinu za kilimo kinachohifadhi maji na rutuba ya udongo kwa wakulima 32 – kilimo hiki kimewezesha ongezeko la mavuno ya mazao mara mbili-tatu zaidi.
- Kwenye vikundi vya kilimo, mradi uliimarisha vikundi vya wakulima wa kilimo hifadhi, vikundi vya wakulima wa miti ya viungo, maharage ya soya, alizeti, mbegu bora za mazao, matunda na mbogamboga n.k.

## Usimamizi wa Maliasili, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

Shabaha kuu ifikapo mwaka 2020 ni pamoja na kuongezeka kwa eneo la misitu ya asili kwa hekta 130,000; angalau miti milioni 100 iwe imepadwa kote nchini



**SHUGHULI MUHIMU**

- hifadhi maliasili
- kulinda, kurejesha na kuhamasisha matumizi endelevu ya rasilimali za mifumo ya kiikolojia ya nchi kavu, hifadhi misitu kwa uendelevu...kupunguza uharibu katika ardhi na upotevu wa bioanuwai.

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Mradi ulifadhili miradi ya uhifadhi wa misitu katika maeneo tisa ya hifadhi kwa kutoa ruzuku kwa ajili ya shughuli za kila siku za uendeshaji – kama vile usafishaji wa mipaka, ukaguzi na uwekaji alama katika mipaka, doria za msituni, uanzishwaji wa barabara na njia za kutembea watalii.
- Shughuli za usimamizi wa misitu zilikwenda sambamba na ushughulikiaji wa visababishi vya uharibifu wa misitu na ukataji miti ovyo kupitia mbinu shirikishi na usaidizi katika shughuli mbadala za kujiingizia kipato.
- Kwa ujumla, shughuli za usimamizi wa misitu na urekebishaji wa maeneo yaliyoharibiwa ulichangia kumea upya kwa msitu kwa kiasi cha hekari 1,000.

## Utalii



**SHUGHULI MUHIMU**

- Kuitangaza Tanzania kwa nguvu zote Tanzania kama ni kivutio cha pekee cha utalii.
- Kuwa na bidhaa mbalimbali za utalii (ukanda wa kusini, kutambua maeneo mapya, utalii wa mambo ya urithi)
- Uboreshaji wa miundombinu (kama barabara)
- Kuboresha mafunzo na uendelezaji wa mbinu.
- Kuhamasisha utalii wa ndani
- Kuboresha mazingira wezeshi kwenye sekta ya utalii.

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Kuimarisha uwezo wa usimamizi wa maeneo ya hifadhi 9 kupitia ufadhili uliowezesha kuweka alama katika mipaka, kusafisha na kupitia upya mipaka, doria za misitu na uzuiaji wa shughuli haramu katika misitu.
- Katika utalii, mradi wa EAMCEF ulisaidia uanzishwaji wa njia za kutembea na barabara za utalii zenye jumla ya urefu wa kilomita 90 katika Hifadhi ya Asili ya Kilombero, kilomita 72 katika Hifadhi ya Nilo, zaidi ya kilomita 50 katika hifadhi za Magamba na Chome, na zaidi ya kilomita 300 katika Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa – ikiwa ni jumla ya zaidi ya kilomita 700 za barabara za kutembea kwa miguu na 177 za kuendesha kwa magari ambazo zote ni muhimu kwa shughuli za utalii.
- Mradi ulifadhili uanzishwaji wa maeneo ya kuweka kambi za watalii 31 katika maeneo ya hifadhi, na pia kusaidia kutangaza maeno hayo kupitia vipindi vya televisheni na redio, pamoja na uandaaji wa vitini vya taarifa na mawasiliano, ikiwa ni pamoja na uanzishwaji na utumiaji wa tovuti.
- Ufadhili wa shughuli mbalimbali katika maeneo ya hifadhi ulichangia katika kuongeza pato la kila mwaka kitokanacho na utalii

## Huduma za upatikanaji wa maji na huduma za usafi wake

Shabaha kuu ifikapo 2020: upatikanaji wa maji salama vijijiji (85%), mijini na Dar es salaam (95%)...



**SHUGHULI MUHIMU**

- uhifadhi na ulinzi wa rasilimali za maji na vyanzo vya maji

**UHUSIANO/NA MCHANGO WA MRADI WA EAMCEF**

- Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki kwa ujumla ulihakikisha kuwa Malindi-maji (catchment areas) yanaendelea kulindwa ikiwamo na mtiririko wa maji katika mfumo mzima wa kiikolojia na maeneo ya jirani.
- Milima ya Tao la Mashariki ni Malindi-maji/vyanzo vya maji kwa mito mingi inayohudumia watumiaji walioko nyanda za chini katika mikoa na miji ya jirani, ikiwamo Jiji la Dar es salaam – maji yanayotumika nyumbani na viwandani kwa asilimia 25 ya wakazi wa miji ya Iringa, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma, na Pwani. Mito mikuu inayopata maji kutoka Milima hii ya Tao la Mashariki ni pamoja na; Ruaha Mkuu, Kihansi, Kilombero, Wami, Pangani, Rufiji na Ruvu.

Andiko hili limeandaliwa kutoka kwenye Ripoti ya Matokeo ya Mradi wa Kuboresha Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania 'Improving Conservation of the Eastern Arc Mountains of Tanzania' (2011-2016), kwa msaada kutoka Serikali ya Norway.

Kwa taarifa Zaidi, wasiliana na: Sekretarieti ya Mfuko wa Uhifadhi wa Milima ya Tao la Mashariki,
Kitalu Na. 348, Eneo la Forest Hill, Barabara ya Kingalu, S.L.P 6053, Morogoro, TANZANIA.
Simu: +255 23 2934274 | Simu: +255 755 330558 | Fax: +255 23 2934273 | Barua Pepe: eamcef@easternarc.or.tz | Tovuti: www.easternarc.or.tz